*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.** BA.8/325/01F/104 **Tarehe:** 17 Novemba, 2021

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA),
S.L.P 9184,
**DAR ES SALAAM**

Kamishina wa Forodha,
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA),
Msimbo wa Posta: 28 Edward Sokoine Drive,
11105 Mchafukoge, Ilala CBD,
S. L. P 11491,
**DAR ES SALAAM**

Mkurugenzi wa Bandari,
Bandari ya Dar es Salaam,
S.L.P 1130,
**DAR ES SALAAM**

Mkurugenzi Mtendaji na Mkurugenzi Mkuu,
Tanzania International Container Terminal Services (TICTS),
S.L.P 71442,
**DAR ES SALAAM**

Mwenyekiti,
Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini (TPSF),
S.L.P 11313,
**DAR ES SALAAM**

Mwenyekiti,
Shirikisho la Biashara na Viwanda (CTI),
S.L.P 71783,
**DAR ES SALAAM**

Mwenyekiti,
Baraza la Wasafirishaji (TSC),
Jengo la Mamlaka ya Bandari Nchini, Sakafu ya 15,
S.L.P 4022,
**DAR ES SALAAM**

Mwenyekiti,
Umoja wa Mawakala wa Meli Tanzania (TASAA),
Jengo la SINOTASHIP- Kurasini,
S.L.P 72457,
**DAR ES SALAAM**

Rais,
Umoja wa Wagomboaji Shehena – Tanzania (TAFFA),
S.L.P 7900,
**DAR ES SALAAM**

Mwenyekiti,
Umoja wa Wamiliki wa Bandari Kavu Tanzania (CIDAT),
Jengo la SINOTASHIP – Kurasini,
S.L.P 70329,
**DAR ES SALAAM**

**YAH: UTARATIBU WA UTOAJI HUDUMA KWA SAA ISHIRINI NA NNE NA SIKU SABA ZA WIKI (24/7)**

**Somo: Utekelezaji wa makubaliano ya wadau**

Tafadhali rejea habari tajwa hapo juu.

2. Wadau wa Sekta ya Usafiri wa Meli wamekuwa wakishauriana kupitia PIC kuhusu namna ambavyo huduma za kibandari zinatekelezwa kwa utaratibu wa saa 24 na siku 7 za wiki (24/7). Katika kufanyia kazi maazimio ya PIC kuhusu suala hili, TASAC iliratibu vikao vilivyokusanya maoni ya wadau kikiwemo kile kilichofanyika tarehe 12/08/2021 katika Ukumbi wa Chuo cha Utalii- Dar es Salaam na hatimaye kulitolea ushauri kwa Katibu Mkuu (Uchukuzi) ambaye ndiye Mwenyekiti wa PIC.

3. Katika kikao hicho, masuala yafuatayo yaliazimiwa kuhusu utaratibu wa kufanya kazi kwa utaratibu wa 24/7:

(i) Utaratibu uendelee kuwa masaa yote 24 kila siku kwenye kuhudumia meli na shehena bandarini na bandari kavu, pamoja na kazi za bandari za kutoa vibali vinavyotakiwa ili shehena bandarini zihudumiwe;

(ii) kuhusu huduma za maofisini zitolewazo na watoa huduma wengine wasio bandari au bandari kavu, masaa yapunguzwe kwa majaribio ya miezi sita (6) kama ifuatavyo;
   a) Jumatatu – Ijumaa: saa 2.00 asubuhi – saa 3.00 usiku;
   b) Jumamosi: saa 2.00 asubuhi – saa 11.00 jioni;
   c) Jumapili na Sikukuu za Kitaifa: saa 3.00 asubuhi – saa 8.00 alasiri; na

(iii) Katika kipindi cha majaribio cha miezi sita, Kanuni zinazohusu utaratibu wa kufanya kazi kwa saa 24 na siku 7 zirejewe ili kutoa tafsiri inayoainisha muda stahiki kwa kila eneo la kazi kwa kuzingatia tija na mahitaji ya Sekta.

4. Kikao cha tano cha PIC kilichofanyika tarehe 29/10/2021 kiliazimia kwamba makubaliano haya yawasilishwe kwa wadau kwa utekelezaji wa kipindi cha majaribio cha miezi sita; Katibu Mkuu (Uchukuzi) ameelekeza azimio hili lianze kutekelezwa.

5. Kwa barua hii, unaelekezwa kuzingatia utekelezaji wa kufanyakazi kwa utaratibu wa saa 24 kwa siku 7 za wiki kuanzia tarehe 01 Novemba, 2021 kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 3 hapo juu.

6. Nashukuru kwa ushirikiano wako.

Moses R. Mabamba
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**

**Nakala:** Katibu Mkuu,
Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi,
Mji wa Serikali Mtumba, 1 Mtaa wa Ujenzi,
S.L.P 638,
**40470 DODOMA.**